# TARGETER WINGS DARASA LA SABA -MWAKA 2021

# MTIHANI WA MJARABU

# KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA

Wings 009

*MUDA: Saa1 dakika 40*

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lililo sahihi.***

Watu wengi___1___unene wa kupindukia na utajiri. Mzazi___2___kuu anapotembea na watoto wake,___3___, ambao hata kutembea vizuri ni kazi___4___. Ulaji wa vyakula___5___sukari na mafuta ___6___unaweza kusababisha maradhi ya moyo na___7___. Wanaopuuza umuhimu wa kutunza afya zao sharti wajiase.___8___wakitaka kuzijua dhiki za hali kama hii wanaweza kuangalia hali ya___9___.

1. A. hupenda B. uhusudu C. hulaani D. hulia
2. A. huona fahari B. huona fedheha C. hupandwa na mori D. hushika mkia
3. A. wapole kama njiwa B. wanono kama kamba C. warefu kama unju D. wanene kama viboko
4. A. yao B. nao C. kwao D. zao
5. A. zenye B. vyenye C. yenye D. chenye
6. A. nyingi B. kingi C. mingi D. mwingi
7. A. ukoma B. bolisukari C. kwashiakoo D. upele
8. A. Usipoziba ufa utajenga ukuta B. Asiyesikia la mkuu huona makuu C. Asiyejua chozi amtazame aliaye D. Asiyejua utu si mtu
9. A. wahadhiri B. waasi C. wahisani D. waadhiriwa

Wazo la kuolewa mapema___10___sana Halima. Alikuwa binti mdogo ndipo tu___11___. Baba yake mwenye itikadi za___12___ alishikilia___13___wake kuwa sharti aozwe. Halima___14___sana na unyama huo uliofanyiwa yeye na wenzake wa___15___ ya kike.

10. A. kulimsumbua B. ilimsumbua C. lilimsumbua D. ulimsumbua
11. A. amebaleghe B. amezaliwa C. amelelewa D. ameelewa
12. A. kisasa B. kijadi C. kitoto D. sasa
13. A. kauli B. sharti C. maoni D. msimamo
14. A. alisikitishwa B. alisikitika C. alisikitikiwa D. alisikitisha
15. A. jina B. namna C. jinsia D. umri

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo.***

16. Udogo wa kauli:
    *'Saa zao hazipendezi mikono'*
    A. kijisaa chake kikononi.
    B. saa yake haipendezi mkononi.
    C. visaa vyao havipendezi vijikononi.
    D. vijisaa vyao havipendezi vikononi.

17. Katika sentensi
    *Embe tamu li jirafuni. "li" imetumikaje?*
    A. Kuonyesha kiambishijina.
    B. Kama kiwakilishi cha ngeli ya LI-YA.
    C. Kuonyesha kiambishingeli.
    D. Kuonyesha wakati uliopita.

18. Kamilisha sentensi hii
    *Mingurumo ya radi ilisikika ________ mvua kunya kwa wingi.*
    A. awali ya B. juu ya
    C. kabla ya D. mbele ya

19. Alama zinazotumika katika hisia na awali ya kuorodhesha vitu huitwaje?
    A. Kihisi, koloni.
    B. Kiulizio, nukta pacha.
    C. Kituo, kipumuo.
    D. Nukta, kimako.

20. Upi si mfupa kati ya maneno haya?
    A. Kitovu. B. Muundi.
    C. Mtulinga. D. Uti wa mgongo.

21. Mjomba ni kakake mama ilhali dadake baba si ________
A. shangazi. B. mbimba.
C. amati. D. halati.

22. Kamilisha sentensi ifuatayo kwa nahau sahihi
*Tangu Tito na kakaye Toti wagombanie kijishamba kile* ________
A. hawajakunja jamvi.
B. hawapaliani moto.
C. hawana kazi wala kazi.
D. hawachezi ngoma goya.

23. Ni methali gani iliyo kinyume na maelezo haya?
*Ukichukua kidogokidogo mwishowe utamaliza.*
A. Chovya chovya humaliza buyu la asali.
B. Bandu bandu huisha gogo.
C. Haba na haba hujaza kibaba.
D. Mchovya asali hachovi mara moja.

24. Kukanusha kufaako kwa sentensi hii ni
*Akimwajiri mtoto atashikwa mara moja*
A. Asingemwajiri mtoto asingeshikwa mara moja.
B. Akimwajiri mtoto asishikwe mara moja.
C. Akimwajiri mtoto hatashikwa mara moja.
D. Asipomwajiri mtoto hatashikwa mara moja.

25. Humu abadani ________ alimoishi panya buku.
A. sipo B. simo
C. siye D. siko

26. Karibu watu wote ni mafisadi nchini
*Neno karibu limetumika kuonyesha*
A. makaribisho. B. nusura.
C. umbali. D. takriban.

27. Mapito amevunja kioo cha gari la mwenyewe
*Neno mwenyewe limetumikaje*
A. Kuonyesha aina ya kitu.
B. Kuonyesha mahali pa kitu.
C. Kuonyesha anayemiliki kitu.
D. Kuonyesha kazi ya kitu.

28. Kitita ni kwa pesa kama vile ushungi ni kwa ________
A. nywele. B. maua.
C. samaki. D. kuni.

29. Bainisha sentensi yenye kiwakilishi cha nafsi ya kwanza
A. Zilimpendeza sana mheshimiwa.
B. Mshipi utakuangusha uumie.
C. Ninamtafuta mwenye gari lililoibwa.
D. Kuku alimkimbiza Sonia jana alasiri.

30. Neno 'bustani' lina silabi ngapi?
A. 7 B. 5
C. 11 D. 4

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Kombo alizaliwa katika familia iliyokula na kusaza. Wazee wake walikuwa na njenje kiasi cha matajiri wengine kuwaita matajiri. Wazaziwe walichukua miaka ayami kumpata mtoto. Hata wakati mwingine walisimangwa na wenzao kuwa walikuwa hawawezi kumpata mtoto kwani walitoa kafara wakapata utajiri badala ya mtoto. Hata hivyo, Mzee Mwinyi na Bibiye Halima walizidi kumlilia Mola ili awajalie mwana. Ama kwa kweli mwomba Mungu si mtovu.

Baada ya miaka kadhaa maombi yao yalijibiwa. Halima alihimili na kukopoa danga la mwana, Kombo. Huyo Kombo naye alikua na kuwa mwana aliyetamaniwa na wote. Kwa vile alikuwa mwana wa pekee, mboni ya jicho lao, wazaziwe walimlea kwa tunu na tamasha. Akaengwaengwa kama yai. Kupendwa huku kupita kiasi kulimvimbisha kichwa.

Kombo aliondokea kuwa mtundu, safihi na kaidi. Alianza mazoea ya kuwaibia wazazi na wanafunzi shuleni. Kila siku, huko shuleni malalamishi yaliendelea na msako uliofanywa haukuzalisha matunda. Zaidi ya hayo, alikuwa akiwakandika vibao wenzake na kuwaumiza vibaya. Mambo maovu yaliyofanywa na kijana huyu yalifunikwa kwa pesa maadam mwalimu mkuu alikuwa sahibu mkuu wa wazazi wake Kombo. Husemwa pesa zilivunja nguu na milima ikalala.

Baada ya mtihani wa kitaifa, Kombo hakufua dafu hata vibaya vibaya. Huo ulikuwa ndio mwisho wa masomo yake. Punde alijiunga na kundi lililomlainisha na kumfunza mapya; kutumia dawa za kulevya. Uraibu lipozidi alianza kuiba vitu vidogovidogo ili kugharamia mahitaji yake kwani wazazi wake walikataa katakata kumpa pesa.

Uraibu wa dawa za kulevya ulikuwa umemnata kama gundi. Mkono wake nao ukazidi kurefuka hadi ukafika kwa majirani. Huko aliiba mbuzi, vikaango, legeni na hata majokofu. Aliweza kuikwepa mitego yote iliyowekwa. Alijinaki na kujifaragua kuwa alikuwa pwaguzi asiye na mpinzani.

Siku moja Kombo alinyemelea chumba cha juu cha ***bahari yao ya nyumba***. Huko ndiko babaye alipokuw akihesabu pesa. Kombo aliusukuma mlango na kuingia ndani. Kombo aliwapata wazazi wake wakihesau pesa. Aliinukia bastola ya baba yake na kumwamuru afungue sefu. Kombo alizichukua pesa zote na kuziweka kwenye shanta na kumfyatulia baba yake risasi moja. Mama yake alipiga kamsa. Askari wapiga doria waliitikia wito. Walimwamuru ajisalimishe lakini akakaidi. Askari mmoja alimfyatulia risasi ya kichwa na punde kimba.

**31.** Kwa mujibu wa aya ya kwanza ni sahihi kusema
A. familia ya Kombo ilipanda kula na kusaza.
B. kwa kawaida matajiri huitana matajiri.
C. Kombo alizaliwa baada ya muda mrefu.
D. wazaziwe Kombo walitoa kafara kupata mali.

**32.** Wazazi wake Kombo walimwomba Mungu ili
A. awajalie mtoto.
B. awajalie mali.
C. awajalie maisha marefu.
D. awajalie mtoto mtu.

**33.** Kulingana na ufahamu, ni sahihi kusema kuwa Kombo
A. alikuwa mtoto wa kipekee.
B. alikuwa mtoto mchapakazi.
C. aliwaenzi wazazi na wenzake shuleni.
D. alikuwa mtoto wa pekee kwao.

**34.** Kilichomharibu Kombo ni nini au nani kulingana na ufahamu?
A. shuleni akaanza wizi.
B. Wazazi wake waliokosea kumrekebisha mapema.
C. Walimu walizidi kumpenda licha ya makosa aliyoyafanya.
D. Marafiki wapotovu waliomfunza wizi.

**35.** Msako uliofanywa shuleni haukuzalisha matunda kwani
A. Kombo alikuwa stadi katika kazi yake.
B. wazazi walimficha mwanawe.
C. walimu walipewa pesa na mwalimu mkuu.
D. Kombo aliwahusisha wanafunzi wengine katika njama yake.

**36.** Baada ya mtihani Kombo hakufua dafu hata vibaya vibaya. Ndiko kusema
A. Kombo alijaribu japo hakupata alama nyingi.
B. Kombo alikuwa kijana mwerevu japo hakupita mtihani.
C. Kombo alikuwa mbumbumbu ambaye alifeli sana katika mtihani wa kitaifa.
D. Kombo hakumaliza masomo ya shule ya msingi kwani alifeli.

**37.** Sababu za Kombo kuviiba vitu vidogovidogo ilikuwa ni
A. kulipia ununuzi wa mihadarati.
B. wazazi wake walimpa pesa kidogo.
C. mihadarati aliyoitumia ilikuwa ghali mno.
D. akiba yake ya benkini haikuwa na pesa.

**38.** Vitu alivyoviiba Kombo kutoka kwa majirai vilikuwa
A. vitaa vya kiufundi.
B. vifaa vya mekoni.
C. vifaa vya shambani.
D. vifaa vya karakanani.

**39.** Maneno 'bahani ya nyumba' ni mfano mzuri wa fani gani ya lugha?
A. Tashbihi. B. Balagha.
C. Msemo. D. Istiara.

**40.** Ni methali gani inayoweza kuelezea taarifa uliyoisoma?
A. Mui huwa mwema.
B. Heri jirani wa karibu kuliko ndugu wa mbali.
C. Mpanda ovyo huvuna ovyo.
D. Ndugu mui heri kuwa naye.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

Nchi ya Pembeni ilikuwa mojawapo ya nchi maridadi zaidi ulimwenguni. Haikuwa na wananchi weng kama yalivyokuwa mataifa mengi. Serikali chini ya uongozi wa Rais Ali Husein ilitenga sehemu kubwa ya ardhi kuwa hifadhi ya misitu. Mbuga za wanyama zilikuwa nyingi. Nchi hii ya Pembeni ilikuwa na ufuko mpana wenye mandhari ya kustarehe. Madini mathalani dhahabu, almasi, shaba, manga, yakuti, zabanjadi, chuma miongoni mwa mengine yalipatikana kwa wingi. Pembeni ilikuwa na milima yenye theluji, mito yenye maji yaliyotiririka hadi baharini, maziwa yaliyojaa samaki pamoja na mabonde yenye majani na nyasi tajiri. Sekta ya utalii ilinawiri kidogo.

Baada ya muda, idadi ya watu ilianza kuongezeka na kuwa ***maradufu***. Watu walipuuza mpango wa uzaz ***uliopigiwa upatu*** na serikali ya nchi ya Pembeni. Sehemu bora za nchi zilivamiwa ili watu wapate makao. Uchun

wa nchi ikaanza kudorora asteaste. Watu hawakuwa na miradi ya kuwaletea pesa. Walianza kuvamia misitu kukata miti kusudi wapate mbao za kuuza. Majangili nao walijihami barabarani na kuanza kutekeleza uhalifu wa Mambo haya yaliiwia serikali ngumu kuyakabili kutokana na uwezo wa vigogo wenye ushawishi mkubwa.

Baada ya kipindi cha miaka kadhaa, nchi ya Pembeni ilipoteza haiba yake. Mvua iliadimika kama barafu ya kukaangwa. Maziwa yalikauka kaukau. Miti ilipukutisha majani na nyasi zikabadilika rangi. Watalii waliomiminika kutoka mataifa mengi walidinda kuitembelea nchi. Vivutio vya watalii vilindindimia na kufifia. Mashambani hakukuwa na chochote cha kuokotwa. Wakulima walipata hasara kubwa.

Maisha yalianza kuwa magumu kuliko jiwe. Ukosefu wa chakula uliwapelekea kula chochote walichokipata. Mkurupuko wa maradhi ya kipindupindu uliwapiga dhoruba. Takribani kila juma mazishi yaliendeshwa kijijini. Hospitali nyingi zilijaa wagonjwa walioponea chupuchupu. Vitoto viliugua utapia mlo. Kina mama na baba walizongwa na njaa isiyo kifani.

Mifugo nao hawakusazwa. Walijifia ovyo. Matatizo tipwatipwa yaliwapokonya raha wananchi wa nchi ya Pembeni. Hapo ndipo mashirika mbalimbali yalipoamua kuwaelimisha waja kwani mambo yalikuwa yameanza kutumbukia nyongo. Serikali nayo ilihiari kuchimba visima na kuwahamazisha raia kupanda miti na kuinyunyizia maji.

Juhudi hizo za serikali za kuhifadhi misitu zilianza kuonekana punde. Mvua ilianza kunya kwa wingi. Watu walikata shauri la kuyaheshimu mazingira yao. Sifa za nchi ya Pembeni zilianza kugonga tena masikio ya walimwengu kwa vishindo vya ndovu aliyejeruhiwa.

**41.** Sababu kuu iliyoifanya nchi ya Pembeni kuwa na ufanisi ni
A. watu walikuwa wachache.
B. misitu ilikuwa mingi na ya kuvutia.
C. watu wote nchini waliwajibika kwa kila njia.
D. serikali tu ndiyo iliyowajibika.

**42.** Vitu vyote vilivyotanjwa kama misitu, mito, milima, madini kwa jina moja huitwa
A. maliasili.
B. mali ya umma.
C. malighafi.
D. mazingira.

**43.** Watalii walifika nchini Pembeni ili kujionea
A. wanyamapori.
B. misitu.
C. utamaduni wa nchi.
D. mandhari na mazingira ya Pembeni.

**44.** Kuongezeka kwa watu maradufu kuliathiri vipi nchi ya Pembeni?
A. Watu walijenga nyumba zao ndani ya misitu.
B. Miundo misingi na maliasili viliharibiwa na watu.
C. Serikali ilipata kipato kidogo kutoka kwa watu ambao hawakuwa na kazi.
D. Watu waliwafukuza wanyama na kupanda miti.

**45.** Neno maradufu lina maana gani?
A. Mara kadhaa. B. Mara chache.
C. Mara mbili. D. Mara nyingi.

**46.** Wananchi wa Pembeni walihariburje maisha yao wenyewe?
A. Kuzaana na kuongezeka sana.
B. Kuingilia misitu na kuikata.
C. Kutusikiliza na kufuata maagizo ya serikali.
D. Kujenga nyumba za kudumu nchini.

**47.** Majangili walitekeleza uhalifu gani?
A. Kuikata miti na kuiuza kinyume na sheria.
B. Kuwaibia watu mali yao.
C. Kuyachafua mazingira kupita kiasi.
D. Kuwawinda wanyamapori bila idhini.

**48.** Tunasema "adimika kama barafu ya kukaanga" Lakini hatusemi adimika kama ________
A. maziwa na tui.
B. kaburi la baniani.
C. maziwa ya kuku.
D. mizizi ya mawe.

**49.** Wagonjwa wa kipindupindu walijaa hospitali Kisawe cha ***kipindupindu*** ni
A. utapiamlo.
B. malale.
C. waba.
D. kichocho.

**50.** Kichwa mwafaka cha taarifa hii chaweza kuwa
A. Mstahimilivu hula mbivu.
B. Mwiba wa kujidunga mtu haambiwi pole.
C. Siku za mwizi ni arubaini.
D. Hasira hasara.